Jarida la Wamama wa Maombi Kimataifa

Huduma ya Wamama ya Kanisa la Umoja Pentekoste

Septemba 2014

Wamama wa Maombi Kimataifa

Sisi ni nani… Wamama wa Maombi wa Kimataifa imeundwa na wanawake duniani kote tangu mwaka 1999. Wanawake hawa hukutana Jumatatu ya kwanza ya kila mwezi kuungana katika maombi kwaajili ya watoto wao na watoto wa kanisa la mtaa na jamii.

Dhamira yetu ... Nia yetu ni kuhifadhi kiroho kizazi hiki na zaidi, pia kurejesha kiroho vizazi vilivyopita

Haja yetu ... Wanawake watakaojiunga pamoja Jumatatu ya kwanza ya kila mwezi kuombea watoto wao**.**

Vipaumbele vitatu vya Maombi ...
1. Wokovu wa watoto wetu (Isaya 49:25; Zaburi 144:12, Isaya 43:5-6).
2. Kwamba wachukue umiliki wa imani katika umri wa kuwajibika (I Yohana 2:25-28; Yakobo 1:25).
3. Kwamba waingie katika huduma ya mavuno ya Bwana (Mathayo 9:38).

Oh, ili nipate kuwa kama mtoto mdogo!

Kathy Streeter

Yesu alisema "... Waacheni hao watoto waje kwangu, wala msiwazuie..." Marko 10:14-15. Katika Mathayo sura ya 18:1-3, wanafunzi walimuuliza Yesu “Ni nani aliye mkubwa zaidi katika ufalme wa mbinguni?” Yesu akamwita mtoto mmoja, akamsimamisha kati yao, kisha akasema, “Nawaambieni kweli, msipogeuka na kuwa kama watoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.”

Hii mistari hutujulisha kwamba watoto ni muhimu sana kwa Bwana. Lakini kwa nini? Ni kitu gani maalum kuhusu watoto wadogo? Kuna sifa nyingi ambazo mara moja huja akilini - wasio na hatia, huamini, imani rahisi, wanafuraha, upendo usio na masharti, husamehe haraka.

Dhidi ya miaka tumekuwa na watoto wengi wa kambo kuishi nasi na wengi wao wamekuwa "watoto wadogo" kati ya umri wa miaka 2-8. Nakumbuka waziwazi watoto wawili walioletwa nyumbani kwetu. Walikuwa ni msichana wa miaka 2 na mvulana mwenye miaka 6. Walikuja wamevaa nguo kubwa labda saizi mbili kuwazidi na hawakuwa na viatu. Watoto walikuwa wachafu na nguo zao zilikuwa zinaota ukungu ndani. Meno ya kijana mdogo yalikuwa yameoza sana hadi kutoa damu usiku na matano kati yao ilibidi kung'olewa. Waliishi katika sehemu mbaya ya mji. Yadi yao ya mbele inaonekana kama jalala. Waliifanya ionekane kama vile walikuwa wanakarakana ya kuuza ili watu wasihisi kuwa wale wanaoingia ndani na nje wanakuja kununua madawa ya kulevya kutoka kwao. Mama yao alikuwa kilema kwa sababu ya ugonjwa wa mifupa na alitembea na kibiongo kama sokwe. Lakini kwa mshangao wangu, kila nikienda kumchukua mama yao kuwapeleka kwa daktari watoto pamoja nasi watoto huwa na furaha kubwa kumuona! Walimpenda bila masharti! Haikujalisha kwamba waliishi katika uchafu na walikuwa na chakula kidogo kula. Haikujalisha kuwa wageni watakuja ndani na nje ya nyumba

yao kununua madawa ya kulevya katika masaa yote ya usiku na mchana. Haikuwa sehemu salama kwa ajili ya watoto na walipuuzwa sana. Lakini wao waliwapenda wazazi wao vivyo hivyo!

Hata kama watoto wote wa kambo walikuwa wametelekezwa, wamenyanyaswa au wamepuuzwa katika namna fulani, wao bado waliwapenda licha ya hali zao. Naamini kuwa hiki ni kile ambacho Yesu alikuwa akizungumzia aliposema msipogeuka na kuwa kama watoto, hamtaingia kamwe katika Ufalme wa mbinguni. Makosa yatakuja lakini ni lazima tusamehe. Maisha si ya haki lakini ni lazima kuweka matumaini. Ni lazima tupende kama Yesu alivyopenda ... pale alipo tuhumiwa uongo, kupigwa na kuchubuliwa. Ni lazima tuwe na uwezo wa kusamehe na kupenda kama watoto wapendavyo ... bila masharti!

Kumbuka: Kathy na mume wake Rick huchunga kanisa la New Life UPC Marshalltown, IA. Yeye ni Rais wa Wizara ya Wamama Wilayani Iowa. Pia anafanya kazi katika shule ya msingi kama paraprofessional na ni mama wa watoto wawili, Tristen, umri wa miaka 13 na Chase, umri wa miaka 12.

Mlee mtoto

Elizabeth Turner

Tulipo funga ndoa kwa mara ya kwanza, mimi na mume wangu hatukujua jinsi gani wazazi wanaweza kulea watoto katika ulimwengu huu mwovu nao kuweza kuwa watu wazuri baadae, hivyo tukajaribu na mbwa wetu! Kweli.

Tuliamua kwamba kama aidha yetu akimwambia mbwa, "Hapana," mwingine haruhusiwi kusikiliza malalamiko ya mbwa. Tutakuwa wa haki, lakini imara. Pia kutakuwa na madhara kwa kutotii. Maisha yetu na mbwa wetu yakawa ya kufurahisha sana.

Muda si mrefu baada ya kuanza mbinu za ufugaji wa mbwa wetu, sote wawili tukaingia kanisani na kuanza kutambua kwamba Biblia ina mpango wa ajabu wa jinsi ya kulea watoto ili waweze, kwa kweli, kuwa watu wema. Na pale Bwana alipotubariki na binti, na kisha kijana, tulikuta kwamba mbinu za ufugaji wa mbwa wetu na taaluma zilihamishiwa vizuri sana na kwa ufanisi!

Hasa cha thamani kwetu katika mradi huu mpya wa uzazi yalikuwa maneno ya busara ya Dada Faith White (mke wa marehemu Kaka Doyle Spears). Alifundisha kwamba tunahitaji kuwajulisha watoto wetu ni tabia gani tunatarajia kutoka kwao na nini adhabu ya kutotii itakuwa. Kisha, kama mtoto akiasi ni lazima kuweka neno letu na kuwapa adhabu iliyo ahidiwa.

Alisema kwamba daima hufuata adhabu kwa kumfanya mtoto amwambie Yesu nini alifanya lililokuwa ni kosa na kumuomba Yesu msamaha. Kisha humchukua mtoto mikononi mwake na kumwambia ni kiasi gani anampenda. Tuligundua hii kuwa njia nzuri ya kuongoza watoto wetu katika njia wanayopaswa waende.

Kitendo kingine cha ajabu Dada White alichoshirikiana nasi ni kwamba kila usiku, baada ya kuweka watoto wao kulala, yeye hurudi na kusimama mlangoni na kuomba kimya kimya kwa ajili ya watoto. Kwa watoto wetu wenyewe, huwa tunasema Sala ya Bwana pamoja wakati tunawalaza, Kaka Turner huwakumbusha kila mmoja wao kukumbuka kwamba Bwana Mungu wetu ni BWANA MMOJA.

Baadaye, napenda kurudi na kutoa maombi yafuatayo kwa ajili ya binti yetu na kisha kijana wetu, nikimaanisha kila sehemu kwa dhati.

Asante, Yesu, kwa ajili ya Rebecca wetu. Weka mkono wako hodari wa ulinzi juu yake na okoa maisha yake mbinguni. Kwa namna yoyote ile, Bwana, okoa maisha yake mbinguni. Tupe hekima ya kumkuza katika namna ambayo yeye mwenyewe atataka kukutumikia Wewe, atakuwa na hamu ya kukutumikia Wewe, naye atakutumikia kila siku ya maisha yake.

Mpe baadhi ya vipaji kutumia kwa ajili ya yako, Yesu, na fanya njia ili aweze kutumia vipaji hivyo kwa utukufu wako.

Mpe chuki ya dhambi, lakini huruma kwa mwenye dhambi. Msaidie kuona ulimwengu huu wa kale wenye uovu kama ulivyo bila kushiriki katika mambo ya ulimwenguni. Saidia haya yote kumfanya akuthamini wewe Yesu, Neno lako, Roho wako, Kweli yako, Watu Wako, na Kanisa lako.

Kama utachelewa kuja kwa muda wa kutosha hata yeye kuolewa, basi naomba kwamba hata sasa uwe unamuinua huyo kijana kukutumikia Wewe pia. Wasaidie kujua kwamba hakuna mtu mwingine anawafaa kwa ajili yao, bali kwamba wao ndiyo sahihi kwao wakati ukifika. Wape uvumilivu kusubiri muda wako kamili, Bwana.

Naomba mtoto yeyote watakaye pata awe baraka kubwa kwa kazi zao kwa ajili Yako na si kizuizi. Tusaidie daima kufanya kazi kama familia kwa ajili Yako, na uwasaidie daima kukutumikia kama familia. Wape kila mmoja wao wito maalum wa kazi kwa ajili Yako, na wape ujasiri, uamuzi, upendo, na mzigo wao hitaji kujitoa kikamilifu kwa kukutumikia Wewe. Katika jina la Yesu, Amina.

Kumbuka: Elizabeth Turner ni mke wa mmishenari William Turner na amesaidia kulea watoto wao wawili, Rebecca, ambaye amekuwa mmishenari wa AIM huko Uturuki na sasa ni mwanachama wa kanisa la UPC huko Columbus, Georgia, na Nathaniel, ambaye ni mmishenari wetu wa UPCI huko Estonia.

Somo la Muhimu Zaidi

Debbie Velie

Nakumbuka kupiga magoti mwishoni mwa benchi la pili kanisani kwetu huko Knoxville, Iowa, nikiomba kwa ajili ya mtoto. Tulikuwa wazi kupitishwa vyovyote vile - Nilicho taka ni mtoto! Tom na mimi tulikuwa tumejadili kupitishwa kabla hatujafunga ndoa. Lilikuwa ni jambo ambalo daima lilikuwa moyoni mwnagu.

Niliwauliza wafanyakazi wenzangu kama kuna anayejua wanandoa wowote mtaani kwetu ambao ni wazazi wa kupitishwa. Walituambia kuhusu wanandoa waliokuwa wamekubali kupitishwa kimataifa. Wao kwa fadhili walikubali kukutana nasi. Tulipokutana na binti yao mzuri, aliyepitishwa kutoka India, tulijua kwamba kupitishwa kimataifa ilikuwa kwa ajili yetu.

Tulipata wakala, tukakamilisha masomo ya nyumbani na kazi nyingi za karatasi na kisha - KUNGOJA - tuliendelea kuomba. Tulichagua Korea na tuliambiwa itachukua takriban miezi sita. Hata hiyo ilionekana kama muda mrefu kusubiri!

Miezi michache baadaye, nilihisi kukata tamaa ya kusubiri, nikachukua siku za likizo kufanya kazi za miradi nyumbani. Wito ulikuja siku hiyo - tulipewa mtoto msichana - kile tu nilicho tumaini. Hatukuweza kungoja hadi Ijumaa kuendesha gari kwenda Des Moines kwenye shirika la kusaini makaratasi kukubali profaili na kuona picha ya mtoto wetu. (Hii ilikuwa ni kabla ya Laptops, skani, na simu za mkononi.)

Wiki chache baadaye, tulikuwa tumesimama katika uwanja wa ndege wa Minneapolis, kwa hamu tukisubiri ujio wa ndege ya Northwest iliyokuwa inamleta mtoto wetu nyumbani. Tuliambiwa kuwa tulivunja rekodi ya kukamilisha kupitishwa kimataifa. Sitasahau kamwe siku hiyo! Walivyo muweka Cori wetu mzuri mikononi mwangu, sikuweza kuacha kulia na niliendelea kurudia, "Mtoto wangu, mtoto wangu." "Nilimwomba anipe mtoto huyu, na yeye alinipa kile nilichomwomba." (I Samweli 1:27).

Miaka mitatu baadaye, tulisubiri katika uwanja huo wa ndege kwa ajili ya ujio wa muujiza mwingine mzuri wa mtoto msichana kutoka Korea, Shaina wetu. Mungu ni mzuri.

Wakati wasichana wangu walikuwa wanakua, niliomba kila siku kwamba Mungu awabariki na wame ambao

watakuwa waaminifu kwa Mungu na kwao. "Na mambo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea" (Mathayo 21:22). Wasichana wote wawili wameolewa kwa vijana wazuri. Na, baraka huendelea kuja. Sasa tuna wajukuu wazuri wanne.

Kamwe sikufikiria kwamba huduma ya maisha yetu siku moja itahusisha kupitishwa. Ni baraka kufanya kazi na mama wazazi jasiri na familia za kuasilisha zenye shauku (tunajua jinsi wanavyojisikia).

Naendelea kuomba kwa ajili ya "watoto wachanga" wangu na familia zao. Omba kwa ajili ya watoto wako kila siku.

Kumbuka: Debbie Velie anaishi Tupelo, MS. Yeye ni mfanyakazi wa leseni ya kijamii na ni Mkurugenzi wa Programu wa New Beginnings (kwa miaka 25). Mke kwa Tom, Mama kwa mabinti wawili wazuri na Bibi kwa wajukuu wanne.

Kutoka kwa Mhariri

Debbie Akers

Mungu anatenda maajabu!

Imekuwa lengo langu na maono tangu mara ya kwanza kuulizwa kuanzisha jarida hili kwamba liwe linapatikana katika lugha mbalimbali. Mungu ni anafungua milango mingi na jarida hili sasa linapatikana kwa Kiingereza, Kihispania, Kifaransa, Kijerumani, Kiholanzi, Kireno, Kirusi, Kigiriki, Kiarabu, Kiajemi, Kicheki, Kichina, Kiswahili, Hungarian na Tagalog. Shukrani za pekee kwa Dada zangu Dianna Tuttle na Jerolyn Kelley na timu ya Watafsiri wanaofanya jambo hili liwezekane kila mwezi! Pia, Mchungaji Don Hanscom anashughulikia kutafsiri katika lugha ya Urdu, Hindi, Thai, Tamil, Kisinhali na Laotian! Hivyo chini ya uongozi wa Dada Gwyn Oakes, Raisi wa UPCI Ladies Ministry, kuwakilisha dhamira yetu ya maombi kwa ajili ya watoto wetu duniani kote bora, kuanzia sasa tutakuwa tukijulikana kama Wamama wa Maombi wa Kimataifa. Tunafuraha na tunazidi kumwomba Mungu aendelee kubariki huduma hii ya maombi. -Debbie Akers, Mratibu na Mhariri wa Wamama wa Maombi wa Kimataifa

Tafadhali tuma shuhuda na mawazo juu ya maombi kwa MothersOfPrayerIntl@aol.com au debiakers@aol.com

Shuhuda

Baada ya kuacha watoto wangu shulen, niliendesha nikizunguka mji wetu na kuomba. Niliomba kwa ajili ya ulinzi wa wangu watoto, kwamba waweze kufanikiwa mwaka huu shuleni, na msimamo wao kwa ajili ya haki uweze kuenea. Inachukua sauti moja tu yenye nguvu kuvutia vijana. Mwanangu alianzisha kampeni ya kuto laani alipoanza shule ya sekondari na sasa wavulana wengine huomba kabla ya kucheza mpira wa kikapu na huomba msamaha kama neno chafu likitoka katika vinywa vyao. Vijana wanaweza kuwa viongozi hivyo wafundisheni watoto wenu kuwa na ujasiri. Baba yangu daima aliniambia, "Kama watu wanaweza kuwa na ujasiri wa kutosha kutenda mabaya, wewe kuwa na ujasiri wa kutosha kutenda haki." Jana Allard

Kutoka Mailbox

Asante dada Debbie Akers, kila mada ni baraka ya nguvu na hekima ninayo hitaji kadri ninavyozidi kukua katika Bwana, Mungu aibariki Huduma ya Wamama!-Shiela T

Amali 31 za Biblia za kuomba kwa ajili ya watoto wako (16-18)

16 Amani kupenda - "Baba., naomba watoto wangu wafanye kila juhudi kutenda yanayoleta amani" (Warumi 14:19)

17 Furaha - "Naomba watoto wangu wajazwe na furaha iletwayo na Roho Mtakatifu." (1 Wathesalonike 1: 6)

18 Uvumilivu - "Bwana, wafundishe watoto wangu uvumilivu katika yote watendayo, pia wasaidie hasa kukimbia na saburi katika mashindano yaliyowekwa mbele yao." (Waebrania 12: 1)

Imewasilishwa na Gwyn Oakes. Hati miliki Bob Hostetler (www.bobhostetler.com). Imetumiwa kwa ruhusa ya mwandishi.

Kwa Mengineyo

Pentecostal Publishing House
Mothers of Prayer Intl
UPCI Ladies Ministries
Reflections
Today's Christian Girl
More to Life Bible Studies
World Network of Prayer
UPCI
My Hope Radio
Multicultural Ministries

Kumbukumbu ya Wamama

Skani msimbo wa QR kwa taarifa juu ya Kumbukumbu ya Wamama

The Girl in the Dress (Msichana katika gauni)..... $10.00
PPH Hisa #: 22690 Lori Wagner

Kitu cha kusisimua! Hatimaye, kitabu kilichoandikwa tu kwa ajili ya wasichana - kitabu juu ya umuhimu na uzuri wa utakatifu. Kitabu hiki kinachoitwa Msichana katika gauni kitatusaidia kutambua ni kwa nini ni muhimu kuchukua msimamo katika dunia ya leo juu ya staha na usafi. Waandishi wamechukua mbinu bora juu ya jinsi Biblia inavyotufundisha kutembea, kuzungumza, na kuvaa.
Mpigie Jane wa UPCI Huduma ya Wamama katika 314-837-7304 X 412 kuweka oda yako leo!!